# HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA PWANI -TUMBI

# JARIDA -TUMBI RRH

**JANUARI 2025** **TOLEO LA KWANZA**



Dkt. Amaani K. Malima

***Kutoka kwa Mwenyekiti,***

Kwa furaha kubwa napenda kuwakaribisha kusoma Jarida letu likiwa ni toleo la kwanza la mwaka 2025.Jarida hili ni Toleo la kwanza katika machapisho ya Jarida la Tumbi ambalo linawapa wasomaji wetu fursa ya kusoma makala mbalimbali za kuelimisha na kufurahisha zinazohusu shughuli zinazofanywa na hospitali.
Kwa kiwango kikubwa Jarida letu linaangazia shughuli za hivi karibuni zilizofanyika katika kipindi hiki 2024 - 2025.

Pamoja na jarida letu hospitali ina tovuti (www.tumbirrh.go.tz),kurasa za mitandao ya kijamii ya facebook, X,pamoja na instagram (hospitali_ya_tumbi),ambazo ni zana mpya, zinazobadilisha mwelekeo wa utoaji na usomaji wa taarifa zetu,na zina umuhimu mkubwa katika kuwaweka karibu wadau wetu.Mwaka huu, tukiwa pamoja na wewe msomaji wetu, tunatarajia kuongeza wafuasi kwenye mitandao ya kijamii ya facebook, instagram, na kuifanya kuwa bora zaidi.Maoni yako, michango na ukosoaji wa kujenga juu ya yote uliyosoma katika jarida letu yamethibitisha kuwa na maana katika kutimiza dhamira yetu ya kutoa na kutengeneza jukwaa bora la habari. Tunatumaini utaendelea kufurahia makala mbalimbali zinazotoka katika jarida hili.Wafanyakazi wetu na wahariri wataendelea kufanya kazi kwa utii na bidii katika kukuletea habari zinazohusu shughuli zote zinazofanywa na hospitali.

## TIMU YA WAHARIRI


Dkt.Amaani K .Maalima - Mwenyekiti
Dkt.Silas Msangi - Mjumbe
Julius Mkama - Mjumbe
Simon A. Lyimo - Katibu
Florence A. Shahanga - Msanifu


*Motto: Your health, our piority*
*“Afya yako, kipaumbele chetu"*

# JARIDA -TUMBI RRH

**JANUARI 2025** — **TOLEO LA KWANZA**

**'SERIKALI YA AWAMU YA SITA IMEENDELEA NA MABORESHO YA MIUNDOMBINU, WATAALAMU NA VIFAATIBA VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA IKIWA NI PAMOJA NA UJENZI WA MAJENGO MAPYA NA VIFAA VYA KISASA'.**



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

*"Idadi ya wajawazito wanaojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya Nchini imeendelea kuongezeka kutoka asilimia 63 mwaka 2021 hadi asilimia 85 mwaka 2023. Lengo la nchi ni kufikia asilimia 95 ya wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ifikapo mwaka 2030".*

## HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA PWANI -TUMBI


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA PWANI TUMBI
S L P: 30041 Kibaha -Pwani, Simu: 0765 106 096
Barua pepe: barua@tumbirrh.go.tz
Tovuti: www.tumbirrh.go.tz


*"Afya yako, kipaumbele chetu"*

# JARIDA -TUMBI RRH

**JANUARI 2025** **TOLEO LA KWANZA**

1

## Huduma za upasuaji




**Katika kuboresha uwezo wa kitaalamu, hospitali ya Tumbi imekuwa ikishirikiana na wataalamu mbalimbali kutoka nchi mbalimbali duniani ili kubadalishana uzoefu na kujengeana uwezo. Kambi ya upasuaji wa watoto (paediatric surgery) zimeendeshwa kwa ufanisi mkubwa kwa ushirikiano wa wataalamu kutoka hospitali ya Tumbi na taasisi ya Ada manes Foundation for children ya nchini Italia ambapo watoto wenye shida kwenye njia ya haja kubwa, mfumo wa mkojo pamoja na henia waliweza kufanyiwa upasuaji huo kwa gharama nafuu.Watoto kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, waliweza kuhudhuria matibabu haya ambayo yalifanyika kuanzia tarehe 08 Oktoba 2024 hadi 17 Oktoba 2024 ambapo watoto 36 walionwa huku 23 kati yao wakifanyiwa upasuaji mkubwa.**

# JARIDA -TUMBI RRH

**JANUARI 2025** **TOLEO LA KWANZA**



**Wataalamu kutoka Taasisi ya Second Chance ya nchini Uswizi wakishirikiana na madaktari wa hospitali ya Tumbi walifanya Kambi ya upasuaji wa kurekebisha viungo (reconstructive surgery) iliyofanyika Machi 2024. Kambi hii ilihusisha watu wenye makovu yatokanayo na madhara ya moto/kuungua, waliozaliwa na ulemavu wa viungo na midomo ya sungura. Wagonjwa hawa walipata huduma hizi za upasuaji kwa gharama nafuu na kurejesha uwezo wa viungo vyao kufanya kazi. Hii ni mara ya saba mfulululizo kutolewa kwa huduma hii katika hospitali yetu.**



**Huduma za upasuaji zinajumuisha upasuaji wa jumla, mdogo na mkubwa, huduma za dawa za usingizi na ganzi, pamoja na chumba cha kutakasa vifaa .**



# JARIDA -TUMBI RRH

**JANUARI 2025** **TOLEO LA KWANZA**

## HUDUMA ZA MAZOEZI TIBA, VIUNGO BANDIA NA VIFAATIBA SAIDIZI



Hospitali ya Tumbi inatengeneza Viungo Bandia na vifaa tiba saidizi kwa kutumia teknolojia bora na mashine za kisasa ambayo inawezesha upatikanaji wa vifaa hivyo muhimu kwa wagonjwa waliopoteza viungo vyao kuweza kurejea kwenye shughuli zao za kiuchumi kama ilivyokuwa awali kabla ya kupoteza uwezo wa kiungo kufanya kazi.

Ni vifaa bora na rafiki kwa wenye tatizo la viungo, walio patwa na ajali au maradhi mengine. Pia mguu huu unaweza kuutumia kuendeshea gari, baiskeli, pikipiki na kutembea kwa haraka zaidi maana ni mwepesi zaidi na mtumiaji hawezi kupata mchubuko wowote.









## MABORESHO MAKUBWA YAFANYIKA KATIKA KUONGEZA UFANISI WA HUDUMA ZA MAZOEZI TIBA, VIUNGO BANDIA NA VIFAA TIBA SAIDIZI









# JARIDA -TUMBI RRH

***HUDUMA ZA MAGONJWA YA AKINA MAMA NA UZAZI***

## Kwa huduma za dharura na usafiri wa haraka kwa mama mjamzito & mtoto mchanga



# PIGA 115 BURE

Zaidi ya dharura 60,000 za wanawake wajawazito, waliojifungua pamoja na watoto wachanga na wanawake wajawazito wamehudumiwa na mfumo wa dharura wa rufaa wa M-mama. Huduma hii inaonesha uhitaji mkubwa sana wa usafiri wa dharura kwa wajawazito, waliojifungua na watoto wachanga ikiwa ni sehemu ya utoaji huduma bora za afya ya mama na mtoto.








# JARIDA -TUMBI RRH

## HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII



## Tumbi yatoa elimu juu ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto

Katika kuadhimisha maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, kitengo cha ustawi wa jamiii katika Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Pwani - Tumbi kwa kushirikiana na ofisi ya Mganga Mkuu wa mkoa wa Pwani kupitia Afisa ustawi wa Jamii Mkoa wa Pwani kimefanya ziara ya kutembelea shule ya msingi na sekondari ili kutoa elimu juu ya masuala ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

Aidha, wataalamu hao walipata nafasi ya kutembelea shule ya sekondari Ruvu Station iliyopo Kibaha na kuweza kuzuia jariobio la ndoa ya Utotoni iliyokuwa imepangwa na wakazi wa eneo hilo wa jamii ya wafugaji dhidi ya msichana wa kidato cha tatu katika shule hiyo.Vilevile waliweza kutembelea makao ya watoto yanayomilikiwa na ubia wa serikali na taasisi binafsi.

Chimbuko la maadhimisho haya limetokana na Tamko la Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa awamu ya saba, Kofi Annan la mwaka 2006 la kutaka Dunia itambue kuwa lipo tatizo kubwa la ukatili wa Kijinsia dhidi ya wanawake na watoto wa kike, hivyo kuna umuhimu wa kuwa na kipindi maalum cha Kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia ambayo ilikubaliwa ifanyike kuanzia tarehe 25 Novemba hadi tarehe 10 Desemba kila mwaka. Lengo la kampeni hii ni kuongeza ushawishi, kubadilishana taarifa na uzoefu, kujenga uwezo wa pamoja, matumizi mazuri ya rasirimali zinazopatikana na kuunganisha nguvu za asasi za kijamii katika kuhamasisha, kuelimisha, kukemea na kuchukua hatua kwa pamoja ili kupinga ukatili wa kijinsia katika jamii.




## URATIBU WA MAONI YA WATEJA



Moja ya majukumu makuu ya kitengo cha Ustawi wa Jamii ni kuratibu maoni ya wateja na kushughulikia malalamiko yao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha uridhikaji wa huduma bora kwa wateja

# JARIDA -TUMBI RRH

***JANUARI 2025*** **TOLEO LA KWANZA**

## HUDUMA ZA UCHUNGUZI WA MACHO



*Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani Tumbi inatoa huduma za uchunguzi wa macho.Kwa sasa tuna wataalamu ambao ni madaktari bingwa kwenye huduma za hizi.*
*Hospitali inaendelea kushirikiana na wadau muhimu ili kuweza kufikia wananchi kwa urahisi na kuboresha upatikanaji wa huduma hizi za afya ya macho kwa maeneo yote.*

**Idara ya macho inatoa huduma zifuatazo;**

- **Kuwaona wagonjwa wote wenye matatizo ya macho**
- **Kutoa Elimu ya afya ya macho**
- **Kupima vipimo vya miwani**
- **Ushauri**
- **Kufanya upasuaji wa mkubwa wa jicho na mdogo hasa mtoto wa jicho**

Mmoja wa wagonjwa walioshiriki kambi ya Macho akifanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho ili kurejesha uoni. Mgonjwa anayehitaji upasuaji wa jicho haitaji tena kupewa rufaa ili kupata huduma kwani inapatikana hapa hospitali ya rufaa ya mkoa wa Pwani Tumbi







# JARIDA -TUMBI RRH

## HUDUMA ZA AFYA YA KINYWA NA MENO

### TOLEO LA KWANZA

### JANUARI 2025

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani Tumbi inatoa huduma za afya ya kinywa na meno,kuweka meno bandia, kusafisha meno pamoja na kutoa elimu hivyo kuwezesha wananchi wa Mkoa wa Pwani na maeneo ya jirani kupata huduma hizo. Huduma hizi zimeboreshwa baada ya ongezeko la vifaa tiba na wataalamu. Hali hil imepelekea wagonjwa wanaohitaji huduma hizi kuongezeka.






# JARIDA -TUMBI RRH

## HUDUMA ZA SIKIO, PUA NA KOO



Matibabu ya sikio, pua na koo) ni taaluma ya matibabu ambayo inalenga katika kutambua, kudhibiti, na kutibu magonjwa ya sikio, pua, na koo

Hospitali ina kliniki ya masikio, pua na koo inayoendeshwa na madaktari wa otolaryngology, wanaojulikana pia kama madaktari wa ENT, ambao wana utaalamu katika kusimamia masuala mbalimbali ya kiafya ikiwa ni pamoja na Magonjwa ya Kawaida Yanayotibiwa katika Kliniki ya ENT(ear, nose and throat)





Afya ya Masikio

- Kupoteza kusikia na tinnitus (mlio masikioni) inaweza kuathiri sana ubora wa maisha yako. Wataalamu wetu wa ENT hufanya tathmini za kina ili kubaini sababu ya kimsingi ya masuala haya na kutoa matibabu yanayofaa, ambayo yanaweza kujumuisha vifaa vya kusaidia kusikia, dawa au upasuaji.
- Wataalamu wetu hutumia mbinu za juu za uchunguzi ili kutambua sababu ya masuala ya usawa na kuendeleza mpango wa matibabu wa kina ili kurejesha kazi ya kawaida.

# JARIDA -TUMBI RRH

## Upatikanaji wa dawa na Vifaa Tiba



Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Pwani Tumbi ni wa uhakika kwa wakati wote. Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba Hospitalini kwa sasa ni asilimia tisini na tano (95%).

Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Pwani Tumbi ina jumla ya vitengo sita vya kutolea huduma za dawa na vifaa tiba, miongoni mwake ni pamoja na stoo kuu ya dawa (Main store pharmacy), duka la dawa la nje (community outlet pharmacy), maduka ya dawa kwenye idara za magonjwa ya nje (OPD), idara ya magonjwa ya akina mama na uzazi, idara ya upasuaji na idara ya huduma za bima. Vitengo vingine ni pamoja na stoo ndogo za dawa na vifaa tiba. Maboresho haya yamesaidia upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kuwafikia wagonjwa kwa kiurahisi na pia kuwezesha utolewaji wa huduma kwa wakati na kupunguza mlolongo mrefu wa kufuata huduma hizo kulingana na jiografia ya hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Pwani -Tumbi.



# JARIDA -TUMBI RRH

## Huduma za kusafisha damu (Dialysis services)




Hospitali ya rufaa ya mkoa wa Pwani Tumbi inatoa huduma zakuchuja na kusafisha damu. Huduma hii ni huduma mpito kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo. Katika hatua hii figo ushindwa kufanya kazi au kuwa na uwezo mdogo wa kusafisha taka mwili hivyo kuhitaji msaada wa mashine maalum ya uchujaji na usafishaji.



# JARIDA -TUMBI RRH

***JANUARI 2025*** ***TOLEO LA KWANZA***

## *Huduma za Maabara*






**Hospitali ya rufaa ya mkoa wa Pwani Tumbi imejiimarisha vya kutosha na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa vya kutolea huduma za uchunguzi ili kubaini tatizo na kuanzisha matibabu sahihi kulingana na tatizo la mgonjwa. Kwa sasa hospitali ya rufaa ya mkoa wa pwani Tumbi inatoa huduma za maabara na uchunguzi wa sampuli za wagonjwa. Hospitali yetu kwa sasa imekidhi vigezo vya kimataifa na kutunukiwa cheti cha ithibati kutoka SADCAS ambacho kinaifanya maabara ya hospitali ya Tumbi kutambulika kimataifa kwa kutoa huduma bora za maabara na utoaji wa majibu ya kuaminika ambayo yanaweza kutumika kimataifa. kwa kutumia ithibati hiyo, maabara ya hospitali ya Tumbi imeweza kupokea na kupima sampuli za vipimo mbalimbali kutoka maabara nyingine ndani na nje ya mkoa wa Pwani jambo ambalo limeongeza idadi ya vipimo vinavyofanyika kwa siku na pia kuongezeka kwa mapato ya hospitali na wakati huo huo, kupunguza usumbufu kwa wagonjwa kufuata huduma hizo maeneo mengine.**

# JARIDA -TUMBI RRH

**JANUARI 2025** **TOLEO LA KWANZA**

## *Huduma za uchangiaji Damu salama*






Kitengo cha Damu Salama hukusanya damu kutoka kwa wachangiaji damu wa hiari (Voluntary-Non Remunerated Blood Donors). kitengo hiki hufanya kazi kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS) -Tanzania ni Programu iliyoanzishwa mwaka 2004 chini ya Wizara ya Afya ambapo una jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zote za usalama wa damu nchini ambazo ni pamoja na upatikanaji wa wachangiaji damu wa hiari, ukusanyaji wa damu kutoka kwa wachangiaji wa damu wanaostahili, uhifadhi wa damu, utengenezaji wa mazao ya damu, upimaji wa magonjwa yaambukizwayo kwa njia ya damu (TTIs), upimaji kwa serolojia ya makundi ya damu na ugavi wa damu salama na mazao ya damu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Mpango wa Taifa wa Damu Salama pia hutoa miongozo kuhusu matumizi sahihi na yafaayo ya damu na mazao ya damu kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

# WAGENI MBALIMBALI WALIO TEMBELEA HOSPITALI YA TUMBI



Timu ya wataalam kutoka taasisi ya ADA MANES FOUNDATION FOR CHILDREN ya nchini Italia ilipofika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Pwani Tumbi kwa lengo la kushiriki kambi ya upasuaji wa watoto(Paediatric surgery) wenye changamoto za njia ya mkojo na mfumo wa haja kubwa, henia pamoja na uvimbe mbalimbali wakiwa kwenye picha ya pamoja na Mganga Mfawidhi wa hospitali ya Tumbi pamoja na timu ya madaktari bingwa wa upasuaji wa hospitali ya Tumbi. Matibabu ya upasuaji wa aina hii ni moja ya maeneo yenye wataalam wachache hapa nchini jambo ambalo hupelekea kufanyika kwa kambi maalum za kibingwa kwa kushirikisha wataalamu kutoka taasisi nyingine kama ambavyo hospitali ya Tumbi inavyoshirikiana na taasisi ya Ada Manes Foundation for Children ya nchini Italia.



Timu yawachezaji wa mpira wa pete chini ya miaka 18 kutoka Nchini kenya walipokuja kuweka kambi kabla kuingia kwenye michezo ya ligi ya michuano kwa klabu zenye wachezaji chini ya miaka 18 walipofika hospitali ya Tumbi ili kufanyiwa vipimo vya uchunguzi



Wanafunzi wanaosomea mchepuo wa sayansi kutoka shule ya Chalinze islamic seminary walipotembelea Hospitali ya Tumbi kwa lengo la kujifunza kwa vitendo kuhusu huduma zinazotolewa katika hospitali ya ngazi ya rufaa ya mkoa

# WAGENI MBALIMBALI WALIO TEMBELEA HOSPITALI YA TUMBI




Watumishi wa hospitali ya Tumbi wakiwa kwenye picha ya pamoja na mratibu wa M-mama Mkoa wa Pwani kutoka taasisi ya Pathfinder International katika kusherekea mwaka mmoja wa utoaji huduma za M-mama Tanzania



Hospitali ya rufaa ya mkoa wa Pwani Tumbi, imeadhimisha sherehe za maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanzania Bara, siku ya tarehe 9 disemba,zilizofanyika kwa kufanya usafi wa maeneo ya kuzunguka hospitali kwa kushirikiana na wataalamu kutoka taasisi mbalimbali zikiongozwa na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani.



*Mwakilishi wa Mkuu wa mkoa wa pwani ambaye pia ni katibu tawala wa mkoa wa pwani akiotesha mti katika Maadhimisho ya Miaka 63 ya Uhuru*



*Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, akiotesha mti wakati wa Maadhimisho ya Miaka 63 ya Uhuru*

## MIUNDOMBINU YA HOSPITALI



Ujenzi wa  (Ramp) njia ya kupandisha wagonjwa kwenda wodi za ghorofani



Eneo la Kuteketeza taka



Mashine ya kufulia nguo za wagonjwa



Kiteketezi taka



# WAGENI MBALIMBALI WALIO TEMBELEA HOSPITALI YA TUMBI




*Wageni kutoka kampuni ya mawasiliano Vodacom Tanzania walipowasili Hospitali ya rufaa ya mkoa wa pwani Tumbi kuadhimisha siku ya huduma kwa wateja duniani(CUSTOMER CARE DAY) walipata nafasi ya kutembelea idara na vitengo na kutoa misaada mbali mbali hivyo kurejesha tabasamu kwa wagonjwa hapa hospitalini katika siku hiyo. Pia katika zoezi hilo Vodacom Tanzania waliweza kushiriki zoezi la kuchangia damu na lengo kuu ikiwa ni kurudisha kwa jamii.Aidha pia timu hii ya vodacom iliweza kuchangia chupa 40 za damu.*

*Ujio wa timu ya wataalamu kutoka taasisi ya Starkeys technologies ya nchini Marekani wakiongozwa na bilionea Austine walipotembelea hospitali ya Tumbi katika kambi ya Upandikizaji wa vifaa vya usikivu.*





MAKAMU WA RAIS WA BENKI YA DUNIA (WORLD BANK)ATEMBELEA TUMBI. Anayesimamia kanda ya Afrika mashariki na kusini Bi. Victoria Kwakwa akiambatana na wadau wa Maendeleo wa M-mama Tanzania ambao ni Vodafone Foundation, Touch Health, Pathfinder International pamoja na Mganga Mkuu wa mkoa Dkt. Kusirye Ukio na Mratibu wa M-mama mkoa wametembelea Hospitali ya rufaa ya mkoa wa pwani Tumbi kwaajili ya kukagua maendeleo ya mfumo wa usafirishaji wa dharura kwa mama wajawazito.waliojifungua na watoto wachanga ndani ya siku 28 wenye changamoto ya kiafya,(M-mama).

# BURUDANI NA MICHEZO



Klabu ya michezo ya hospitali ya Tumbi ikifanya mazoezi ya pamoja



Tumbi jogging club wakishiriki mbio za NBC marathon jijini Dodoma ambapo Waziri Mkuu alikuwa Mgeni rasmi.



Tumbi jogging wakishiriki mbio za Coastcity Marathon kibaha Pwani



Tumbi jogging wakishiriki mbio za CRDB Marathon Jijin Dar es salamaa



Tumbi jogging wakishiriki mbio za CRDB Marathon Jijin Dar es salamaa ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Naibu waziri mkuu na waziri wa Nishati Mhe Dkt. Dotto Biteko

## VIPAUMBELE VYA BAJETI YA WIZARA YA AFYA 2024/25



**MHE. JENISTER MHAGAMA**
**WAZIRI WA AFYA**



**DKT. GODWIN MOLLEL**
**NAIBU WAZIRI**

1. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa
2. Kuimarika upatikanaji na ubora wa huduma za afya ngazi ya Zahanati hadi Taifa
3. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini
4. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtotona watoto wachanga;
5. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika sekta ya Afya
6. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi
7. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala
8. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za magonjwa ya kuambukiza, yasiyoambukiza na mlipuko
9. Kuimarisha huduma za afya ya akili, utengamao na ulemavu
10. Kusimamia Tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti za afya

**KARIBUNI KWA HUDUMA ZA UCHUNGUZI, USHAURI NA MATIBABU**

*"Afya yako ,kipaumbele chetu".*

**TUNAPATIKANA KIBAHA MJI,PWANI**

**HUDUMA ZETU NI SAA 24 KILA SIKU,**
**TUNAPOKEA BIMA ZA AFYA ZIKIWEMO NHIF, STATEGIES, JUBILEE, ICHF PAMOJA NA WCF.**